**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA**

*Barua zote ziandikwe kwa:*
*Mkuu wa shule*
*Simu:* Mkuu wa shule 0764818574
*Barua pepe*: lolezagirls@gmail.com

***Kumb.Na.LOL/MCH/563/2022/VOL.II/193*** **Tarehe: 18.04.2024**
**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi,**
**...............................................................................**
**...............................................................................**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI LOLEZA, HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA, MKOA WA MBEYA MWAKA 2024/2025**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano (V) katika shule hii mwaka **2024/2025** na atasoma tahasusi ya.................. Shule ya Sekondari Loleza ipo umbali wa kilomita moja (1) kutoka stendi kuu ya mabasi yaendayo Mikoani, na inapakana na Hospitali ya Kanda ya Rufaa Mbeya. Usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana kwenye Stendi kuu ya mabasi yaendayo mikoani na nauli ni shilingi mia nne (400/=),kwa bajaj shilingi 800/= na kwa pikipiki shilingi 2000/=
Muhula wa mosomo unaanza tarehe .........,hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **............** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **.............**Endapo mwanafunzi atachelewa kuripoti; nafasi yake itachukuliwa na wanafunzi wengine.
Mzazi/mlezi na mwanafunzi, mnatakiwa kusoma/kujaza maelekezo hayo kwa umakini, ili kuepuka usumbufu siku za baadaye.
**Ni mategemeo yangu makubwa kwamba Mwanafunzi atasoma kwa bidii, atatoa ushirikiano kwa wenzake, Walimu na Watumishi wengine na atazitii Kanuni na Sheria za Shule katika kipindi chote awapo Shuleni ili kuleta Ufanisi na maendeleo ya Shule**.

**“JUHUDI NA MAARIFA NI SHINA LA MAENDELEO” Ndiyo kauli mbiu ya Shule hii, tafakari na tumia nafasi hii kwa manufaa yako na Taifa kwa ujumla.**

________________________
TUMTUKUZE ELIA MPINDO
**MKUU WA SHULE**

**SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.**

Shule inaendeshwa Kwa mujibu WA Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na Sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake pamoja na maelekezo ya kujiunga na shule hii. Mambo hayo ni pamoja na:

**A : HESHIMA**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1. Kusimama na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote aliyewazidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
2. Kutotumia lugha mbaya, wakati wowote kati yao wenyewe, kwa walimu na kwa watu wengine.
3. Kuwaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wake.
4. Kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wenzake katika kazi.
5. Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote.
6. Kuwa na kucha fupi zisizopakwa rangi na nywele fupi pia ziwekwe katika hali ya usafi kila wakati, kuvaa mavazi ya heshima.
7. Kuitika mara moja na kukimbilia aliko Mkuu anayekuita.
8. Kuheshimu bendera ya serikali, picha za viongozi wa serikali, nembo ya Taifa “coat of Arms”, wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
9. Kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa kulia chakula, ofisi za shule, mali ya binafsi na mali ya umma.
10. Kusimama katika mstari wakati wa kupokea huduma.
11. Kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote ulipo.
12. Kunyosha mkono juu na asimame anapouliza na kujibu maswali.
13. Kukaa kimya wakati wote anapokuwa darasani, asitoke bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko.
14. Kuheshimu na kukubali tofauti za kisiasa, kidini na kiutamaduni zilizopo katika jamii.
15. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.
16. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
17. **Ni marufuku kwa mwanafunzi kuleta** vifaa vifuatavyo shuleni **SIMU au KIFAA CHOCHOTE CHA SIMU, Pasi ya umeme, Camera, “Heater”, Smart Watch,** pamoja na **VYAKULA** vya aina yoyote na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza vifaa tajwa hapo juu.

**B: MAHUDHURIO**

Kila mwanafunzi anatakiwa:

1. Kuhudhuria shule muda wote wa masomo.
2. Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.
3. Kuhudhuria katika kazi zote za mikono.
4. Kuhudhuria mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa, mikutano ya nyumba na madarasa.

**C: MAANDALIO YA JIONI**

1. Kila mwanafunzi anatakiwa ahudhurie maandalio ya asubuhi na jioni kuanzia Jumatatu hadi jumapili saa 1.30 hadi saa 5.00 usiku. **Mwanafunzi harushusiwi kukaa au kulala bwenini muda huu ukipatikana adhabu kali itatolewa dhidi yake.**
2. Ili kufanikisha maandalio ya jioni na asubuhi mwalimu wa somo atakuwa anatoa kazi na kuhakikisha kuwa kazi hizo zimefanywa.

3. Walimu wa zamu watakuwa wanasimamia maandalio ya asubuhi na jioni jioni kikamilifu.

**D: MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1. Wizi
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro/kulala nje ya shule bila ruhusa
3. Kugoma na kuhamasisha mgomo
4. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
5. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
6. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
7. Uvutaji wa sigara
8. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
9. Kupata ujauzito au kutoa mimba
10. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yeyote yale yanayovunja sheria za nchi.
11. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
12. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
13. Kudharau bendera ya taifa.
14. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
15. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**a. MAENDELEO YA MWANAFUNZI KITAALUMA NA TABIA.**

**SHULE INA UTARATIBU WA KUTUMA/KUMKABIDHI MWANAFUNZI TAARIFA ZA MAENDELEO YA MWANAFUNZI KITABIA NA KITAALUMA YA KILA MUHULA ANAPORUDI NYUMBANI/LIKIZO, TAFADHALI MZAZI/MLEZI HAKIKISHA UNAIPATA NA KUMSHAURI MWANAO KUHUSU MAENDELEO YAKE NA MZAZI ATATAKIWA KUTOA MAONI YAKE KUHUSU MAENDELEO YA MTOTO NA KUYARUDISHA SHULE.**

**b. KUWAHI.** Kila mwanafunzi anatakiwa:

1. Kuthamini muda.
2. Kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku.
3. Kufika/Kuripoti shuleni kwa tarehe zilizopangwa kufuatana na muhula husika na muda husika.

**c. SARE YA SHULE.** Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare ya shule wakati wote wa:

1. Masomo darasani
2. Kutoka nje ya shule Kwa shughuli za kishule.
3. Baraza la shule.
4. Kwenda hospitalini.
5. Kwenda maandamano.
6. Wanaposafiri kuja shuleni au kwenda makwao wakati wa likizo.
7. Kazi za mikono (vazi la kazi).
8. Michezo (Vazi la Michezo)

**NB: MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUJA NA NGUO ZA NYUMBANI NJE YA ZILE ULIZOAGIZWA NA SHULE AU KUVAA KOFIA, MIZURA, KUFUGA KUCHA NDEFU, KUPAKA RANGI KUCHA NA MIDOMO, KUVAA HELENI, MIKUFU, BANGILI, NGUO ZA KUBANA, VIATU VYENYE VISIGINO VIREFU, MAPAMBO MENGINE YOYOTE PAMOJA NA SARE AKIWA SHULENI.**

**d. MIPAKA YA SHULE.** Kila mwanafunzi azingatie mipaka ya shule kama ifuatavyo:

1. ***NI KOSA KWA MWANAFUNZI KUTOKA NJE YA MIPAKA YA SHULE BILA KIBALI CHA MKUU WA SHULE. UKITOKA SHULE BILA KIBALI NI UTORO UTAKAOSABISHA KUFUTWA SHULE.***
2. Kutotembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum:
   - i. Chumba cha walimu (staffroom).
   - ii. Ofisi za shule.
   - iii. Maabara.
   - iv. Jikoni.
   - v. Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

**e. UGONJWA**

1. Tafadhali mzazi/mlezi unatakiwa kufanya **uchunguzi wa kina wa Afya ya mwanao kabla hajaripoti** shuleni na wakati wa likizo ili kuepuka usumbufu wakati wa masomo.
2. **Mwanafunzi mwenye matatizo ya kiafya lazima aufahamishe uongozi wa shule au matron wa shule Kwa uwazi**, mara afikapo shuleni ili iwe rahisi kumhudumia mara apatapo changamoto. **WAGONJWA WAJE NA VYETI KUTOKA HOSPITAL ZINAZOTAMBULIKA.**
3. Endapo kutakuwa na tatizo lolote la kiafya kwa mwanafunzi awapo shuleni, mwanafunzi atatakiwa kutoa taarifa kwa mwalimu wa zamu, mwalimu wa darasa, kwa matroni wa shule, mwalimu mlezi n.k. mwanafunzi harusiwi kutunza dawa yoyote bwenini. Dawa zote zitunzwe kwa matroni/Nesi wa shule.
4. Mwanafunzi mgonjwa ataruhusiwa kupumzika katika zahanati ya shule na endapo atazidiwa atapelekwa katika hospitali ya serikali.
5. **Shule haitoi chakula maalum (special diet) kwa wanafunzi wagonjwa.**

**ANGALIZO KWA MWANAFUNZI**

1. Mwanafunzi haruhusiwi kuandika maandishi katika dawati, meza, viti, vitabu au kwenye kuta za majengo ya shule.
2. Ni kosa kwa mwanafunzi kujihusisha au kukutwa na kitu chochote kinachohusisha mapenzi **mfano barua, daftari lenye nyimbo za mapenzi n.k.**
3. Ni kosa kwa mwanafunzi kupita eneo lisilo na barabara maalumu au kutupa takataka maeneo yasiyo rasmi au kuziona takataka bila kuziondoa, hii ni kwa ajili ya kutunza mazingira ya shule.
4. **Ni kamwe, na hairuhusuwi wanafunzi wawili kulala kitanda kimoja, na kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa(Kitanda kimoja kwa mwanafunzi mmoja tu).**
5. **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. ( Msiba au Ugonjwa).**

**f. BIMA YA AFYA**

***KILA MWANAFUNZI MWENYE BIMA YA AFYA ATATAKIWA KUJA NAYO ili kuepusha gharama za matibabu zinazoweza kujitokeza pindi mwanao atakapopata changamoto ya kiafya.***

**A. MAVAZI PAMOJA NA SARE**.

Sare za shule hii;

1. Sketi ndefu mbili (02) rangi ya bluu bahari**–light blue (kitambaa cha suti namba moja)**.
   **Mshono:**
   ***Urefu wa sketi unatakiwa ufike kwenye kifundo cha mguu (Ankle) isiyobana mwili yenye malinda 12 ya mfukuzano (malinda sita (6) mbele na sita (6) nyuma. Iwapo kuna changamoto yoyote itajitokeza ya ushonaji, rangi halisi ya kitambaa pamoja Na mtindo WA ushonaji, fika shule kwa maelekezo zaidi. (Sketi ufundi kushona sh. 6000, na gauni sh.7000 karibuni tuwahudumie).***
2. Mashati mawili mikono mirefu rangi nyeupe (aina ya tomato)
3. Track suit rangi ya bluu bahari zisizo bana mwili na T-shirt aina ya '**form six' yenye kola** rangi ya bluu bahari pamoja na raba za michezo.
4. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi (pair mbili), na soksi nyeupe za kutosha nzito zisizo na maua. **USIJE NA SOKSI NYEUSI**
5. **Pull-neck** nyeupe mbili pamoja na nyeusi mbili ambazo hazina urembo wowote (plane)
6. **Masweta mawili** rangi ya bluu bahari (light blue) - **Sweta lolote la nyumbani halitakiwi.**
7. Nguo za kushindia - gauni (shamba dress) zinatakiwa mbili (02), mikono mifupi, yenye urefu mpaka kwenye kifundo cha mguu (ankle), mshono wa solo, shingoni iwe "round" rangi ya **"DARK BLUE" – kitambaa cha suti namba moja.(ufundi kushona shuleni tshs.7000).**
8. Vitenge viwili na taulo
9. Mashuka mawili rangi ya bluu bahari na jeupe moja (01) la kutandika lisilo taliziwa maua yeyote.
10. Blanketi moja zito na chandarua- rangi nyeupe.

11. **MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUSUKA NYWELE.**

**NOTE: KWA WANAFUNZI WA DINI YA KIISLAMU**

1. **Alete hijabu mbili (04), mbili** zenye rangi nyeupe kwa ajili ya kuvaa awapo darasani, na nyingine mbili zenye rangi nyeusi kwa ajili ya kushindia. HIJABU ZOTE **ZISIWE NA UREMBO WA AINA YOYOTE NA ZIFUNIKE KIFUA CHA MWANAFUNZI TU (ZISIFUNIKE TUMBO) NA PIA IWE NDEFU KUFIKIA KIWIKO CHA MKONO AKISIMAMA, NA SI VINGINEVYO**
2. Baibui **moja (01)** nyeusi na juba rangi ya udongo (chocolate) **zisizo na urembo wa aina yoyote za kuvaa wakati wa kuswali.**

**B. MICHANGO SHULE YA BWENI.**

**a.** Mchango wa uendeshaji wa shule elfu sitini na tano (65,000/=) tu;

i. Tahadhari elfu tano (5,000) tu hairudishwi

ii. Nembo elfu tano(5,000/=) tu

iii. Kitambulisho cha shule elfu tano (5,000/=) tu

Michango tajwa hapo juu jumla 80,000/= ilipwe kupitia benki ya NMB


Jina la Akaunti: **HEADMISTRESS LOLEZA SECONDARY SCHOOL**

**Akaunti Namba: 61003500144**

iv. Shilingi 10,000 kwa ajili ya kukodisha godoro Kwa mwaka. (**Magodoro yanapatikana shuleni na hatupokei godoro lolote kutoka nje ya shule)**. **Fedha hii tu** ilipe kwenye account number **61010016118 NMB (HEADMISTRESS LOLEZA SEC. SCHOOL - MIRADI)**

Mwanafunzi anatakiwa kuja na risiti Halisi za malipo ya benki **(ORIGINAL PAY IN-SLIPS).**

**Hapa chini ni mfano wa ujazaji wa fomu ya kuweka fedha benki.**



NMB

NATIONAL MICROFINANCE BANK PLC
AGENCY BANKING - NMB WAKALA
CASH DEPOSIT / WITHDRAWAL SLIP
FOMU YA KUWEKA / KUTOA FEDHA TASLIMU

Agent Number/**Namba ya Wakala**

Date/**Tarehe** 15/07/2017

Account Number
**Nambari ya Akaunti** 6110035000144

Account Name
**Jina la Akaunti** HEADMISTRESS LOLEZA SECONDARY SCHOOL

Deposit/**Kuweka**

Withdrawal/**Kutoa**

Account Figures
**Kiasi kwa Tarakimu**

TZS 168,000/=

Amount in Words/**Kiasi kwa Maneno** LAKI MOJA NA ELFU SITINI NA NANE ELFU

| Denomination/ Mnyambulisho | Number of Notes/ Idadi ya noti | Amount/ Kiasi |
|---|---|---|
| 10,000x | 16 | 160,000/= |
| 5,000x | 1 | 5000/= |
| 2,000x | 1 | 2000/= |
| 1,000x | 1 | 1000/= |
| Coins / Sarafu | | |
| TOTAL / JUMLA | | 168,000/= |

Purpose/**Kwa ajili ya:** ADA NA MICHANGO MINGINE

Transaction ID / **Kumbukumbu ya Muamala**

Agent location / **Wakala Eneo**

Depositor's Name / **Jina la Mweka Fedha** AGNES JOHN

Depositor's Phone / **Namba ya simu ya Mweka fedha**

Agent's Signature and Stamp **Saini na Mhuri wa Wakala**

Depositor's Signature / **Sahihi ya mweka fedha** A. John

This form will be valid only if signed by the customer, countersigned by Agent.
**(Fomu hii itakuwa sahihi iwapo itakuwa na maelezo na saini ya mteja, na saini ya Wakala)**
02-10-017

## C. MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI

1. **REAM mbili (02) kwa pamoja** za karatasi **$A_4$ (kwa mwaka), ISIPOKUWA WANAFUNZI WA MCHEPUO WA PCM WALETE REAM MOJA (01) YA KARATASI $A_3$.**
2. Madaftari makubwa (counter books angalau three quire) zisizopungua 12 (dazani moja)
3. **Dissecting kit** kwa wanafunzi wa mchepuo wa **CBG na PCB**
4. Scientific Calculator kwa Wanafunzi wa Masomo ya Jiografia na Sayansi
5. Oxford - Advanced Dictionary hasa kwa wanafunzi wanaosoma somo la kingereza.
6. Vyombo vya chakula **(sahani, bakuli, kijiko na Kikombe),** Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko kwa matumizi binafsi.
7. **TRANKER MOJA DOGO NA BEGI DOGO LA KUWEKEA DAFTARI**
8. **"Spring file" (lisiwe la plastic) moja (01)** lenye rangi iliyotajwa, **CBG** – rangi ya Njano, **PCB** – rangi ya blue, **HKL** – rangi ya Kijani, **HGL**- rangi ya Blue**, HGK** – rangi pink,na **PCM** rangi ya Pink kwa ajili ya kuhifadhia nyaraka za mwanafunzi.
9. Mkebe (mathematical set),peni za kutosha,penseli na rula
10. **Alete pasport size tatu (3)** pazia la light blue (blue bahari) nyuma na avae shati la shule/nyeupe kwa ajili ya kuweka kwenye faili litakalo hifadhi nyaraka za mwanafunzi.

**VIFAA VYA USAFI**

**Note;** Kila mwanafunzi atapaswa kuja na **Mfagio Mmoja (01) aina ya chelewa** pamoaja na vifaa vingine kama vilivyoanishwa kwa kila Tahasusi hapa chini.

1. CBG– Squeezer (01), Kizolea taka (01), Soft Broom (01),na Brush ngumu ya kusugulia sink la choo (Tanzanian type)-01.
2. PCB–Jembe lenye Mpini (01) na Brush ngumu ya kusugulia sink la choo (Tanzanian type)-01, Siko (01),
3. PCM– Spade (01), Rake kwa ajili ya kukwangua taka (01)
4. HGL– Panga (01), hard broom (01),ndoo lita 10 (01) na kwanja (01)
5. HKL– Sululu na Mpini wake (01), Soft broom (01) na Ndoo lita 20 (01).
6. HGK– Jembe na Mpini wake (01), Mkasi wa Kukatia Maua (01), Ndoo lita 20 (01)
7. HGFa – kwanja (fyekeo) (01), harbroom (01), panga na ndoo lita 20 (01)
8. HGLi – Siko (01), Spade (01), soft broom, ndoo 01 ya lita 10.

| MUHIMU: MWANAFUNZI AJE NA NAKALA YA HATI YA MATOKEO (RESULT SLIP) YA KIDATO CHA NNE |
|---|

**ANGALIZO KWA MZAZI/MLEZI**

1. Mwanafunzi hataruhusiwa kwenda benki/posta/kituo cha mabasi kuchukua fedha au mzigo zitakazotumwa Kwa njia hizo.
2. **Mtoto akishapokelewa shuleni**, Mzazi/mlezi au ndugu yeyote yule haruhusiwi kuja kumwona labda uitwe na uongozi wa shule, kwa maana nyingine **"HAKUNA SIKU YA KUWATEMBELEA WANAFUNZI"**
3. Mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mtu wa nje ya shule yafanyike tu kupitia Uongozi wa shule.
4. Mwanafunzi aripoti shuleni akiwa ameva **sare ya shule asije na nguo yoyote ya nyumbani zaidi ya mavazi yaliyoagizwa hapo juu.**
5. Barua ya mwanafunzi itakayotiliwa wasiwasi itafunguliwa na Uongozi wa shule.
6. Ni marufuku mwanafunzi kuwa na kutumia pasi ya umeme ama kifaa chochote kinachotumia umeme.

**MAWASILIANO KATI YA MWANAFUNZI NA MZAZI/ MLEZI - PALE INAPOBIDI**

1. Mwl. Mbalwa, Umilila - Makamu Mkuu wa Shule - **0758267648 / 0763040297/0769167075/ 0712680186 / 0789438196**
2. Elizabeth Mjema – Malezi **-0765806147, 0786007905**
3. Mwl. Zablon, Neema.K - Malezi - **0755841048 / 0784905133**
4. **Mwl.Atukuzwe kabuje -Taaluma – 0687852203, 0656035149,0763025722**

**Mzazi/Mlezi ukitaka kutuma fedha ya matumizi ya mwanafunzi kupitia namba hizo kumbuka kuandika ujumbe au kupiga simu kumtambulisha mhusika aliyetumiwa, MFANO: NIMETUMA SHILINGI 30,000/= KWA AJILI YA MWANAFUNZI VERONICA JAMES FORM FIVE CBG kupitia kwa Juma Hamisi. HII NI KWA FEDHA ZA MATUMIZI TU**

**MWANAFUNZI HARUSIWI KUJA NA SIMU SHULENI, ATATUMIA SIMU ZILIZOPO SHULE KWA UTARATIBU MAALUM.**

**NB: MZAZI/MLEZI EPUKA KUTAPELIWA NA WEZI**. Tii yafuatayo,

1. Usitume fedha kwa mtu USIYEMFAHAMU - atakayekupigia au kukuandikia ujumbe kuwa yeye ni mwalimu na kwamba yupo na mwanao/mwanafunzi hospitali anaumwa sana au ameanguka ghafla na kuvunjika. **KWA MSAADA ZAIDI WASILIANA NA WAHUSIKA TAJWA HAPO JUU KWANZA AU MKUU WA SHULE**.
2. Ukitumiwa ujumbe unaohitaji utume pesa kwenye namba ya simu usiyoijua upuuze ujumbe huo.

**TAARIFA BINAFSI (IJAZWE KIKAMILIFU NA IRUDISHWE SHULENI)**

1. Jina lako kamili kama lilivyotumika kidato cha nne…………………………………………….
   Dini yako/Dhehebu………………………………………………………………………………
2. Jina kamili la baba mzazi/mlezi: ………………………………………………………………..
   Kazi yake…………………………………………………………………………………………
   Anwani kamili ya baba mzazi/mlezi …………………………………………………………………………………….
   Na. yake ya simu ya mkononi…………………………… Na. yake ya simu ya mezani……………………………...
   Mahali anakoishi baba mzazi/mlezi: Mkoa…………………. Wilaya…………….. …………
Tarafa……………………………… Kijiji/Mtaa……………………………
3. Jina kamili mama mzazi/mlezi…………………………………………………Kazi yake…………………………………………………
   Anwani kamili ya mama mzazi/mlezi………………………………………………………………………………………….
   Na. yake ya simu ya mkononi…………………………………………………………….Na. yake ya simu ya mezani ……………………………
   Mahali anakoishi mama mzazi/mlezi: Mkoa………………… wilaya……………
   Tarafa…………………………………… Kijiji/Mtaa……………………………..

4. **MAJINA YA WATU WATANO WANAORUHUSIWA KUMCHUKUA MTOTO WAKO BAADA YA KUITWA NA UONGOZI WA SHULE. (KUMBUKA HAKUNA SIKU YA KUWATEMBELEA WANAFUNZI)**

| Na | Jina lake | Uhusiano | Mahali anakoishi | Anwani na namba yake ya simu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5 | | | | |

5. Shule nilizosoma msingi hadi kidato cha NNE.

| Na | Jina la shule | Darasa/Kidato | Kuanzia mwaka hadi mwaka | Mkoa | Wilaya | Kijiji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | | |
| 2. | | | | | | |
| 3. | | | | | | |
| 4. | | | | | | |
| 5. | | | | | | |
| 6. | | | | | | |

Namba yangu ya mtihani wa kidato cha nne………………..

6. Matokeo yangu ya mtihani wa kidato cha nne.

| Na | Somo | Daraja | Na | Somo | Daraja |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | 6 | | |
| 2. | | | 7 | | |
| 3. | | | 8 | | |
| 4. | | | 9 | | |
| 5. | | | 10 | | |

Nilipata divisheni………………….. Pointi……………..

7. Tarehe niliyoripoti hapa Loleza sekondari ni ………………………..

Masomo nitakayosoma ni:

1. ……………………………. ……… 2. ………………………………… 3.…………………………………

4. ……………………………………. 5. ………………………………...................

1. Matarajio yangu baada ya kumaliza kidato cha sita ni:
2. ……………………………………………………………………………………………..............................
.
3. ……………………………………………………………………………………………..............................
.
4. ……………………………………………………………………………………………..............................
.
5. Hapa shuleni ningependa nijiunge na:
    1. Michezo: (i) ……………………….. (ii) ……………………… (iii) ………………………...
    2. Kikundi cha utamaduni wa………………………………………………………………..
    3. Mradi wa……………………………………………………………………………...

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

MKOA WA ……………………………………..

OFISI YA MKUU WA WILAYA,
Wilaya ya …………………..
S.L.P…………………..
TAREHE……………………

Mkuu wa shule,
………………………………………
………………………………………
……………………………………….

**UTHIBITISHO WA URAIA WA TANZANIA**

Nathibitisha kuwa ………………………………………………………………….. (Jina kamili la mwanafunzi) ni raia wa Tanzania kwa kuzaliwa/kwa kuandikishwa.

Baba yake (Jina kamili)……………………………………………………………….

Amezaliwa katika Mkoa wa ………………………………………………Wilaya ya ………………………………………….

Tarafa ya …………………………………………………Kata ya ………………………………………

Mama yake (Jina kamili)……………………………………………………………………………

Amezaliwa katika Kata ya …………………………………………..Wilaya ya ……………………………………………….

………………………………………………. ……………………………..
**SAINI YA MKUU WA WILAYA** **MHURI**

**NB:** Kila mwanafunzi analazimika kuishughulikia hati hii kikamilifu. Ikishajazwa irudishwe kwa Mkuu wa Shule siku ya kuripoti shuleni kwa wale wasio na Cheti cha kuzaliwa. **AU LETA NAKALA YA CHETI CHA KUZALIWA BADALA YA FOMU HII.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA JIJI MBEYA-SHULE YA SEKONDARI LOLEZA**

## FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE HII

1. **Sehemu ya mwanafunzi.**

**A. KUJIUNGA NA SHULE HII**

Mimi ……………………………………………………………… ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha kwanza/tano mwaka……………………..katika Shule ya Sekondari ya Loleza na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na nchi. **Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za Elimu ya kujitegemea**

**B. KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

Mimi ………………………………. ….mwanafunzi wa kidato cha tano, mchepuo wa/tahasusi ya ……….. Ninaahidi mbele ya mzazi/mlezi na familia yangu kwa ujumla, kuwa sitashiriki au kuchochea fujo, mgomo na makosa ya jinai kwa muda wote niwapo shuleni na nyumbani nitakuwa raia mwema na mzalendo kwa nchi yangu.

**Saini ………………………… tarehe …………………………**

Anuani yangu ya kudumu ni …………………………………………………..

…………………………………………………..

…………………………………………………..

2. **Sehemu ya mzazi/mlezi.**

Mimi ………………………………………………… ninakubali mtoto wangu ……………………………………………. kusoma katika Shule ya Sekondari ya Loleza mwaka ………………………………… Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Aidha ninaahidi nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na taifa. Na nitafuatilia Maendeleo yake Kitaaluma, tabia na mwenendo nidhamu ya mtoto wangu nikishirikiana na walimu.

Anuani yangu ya kudumu ni ……………………………………………………………

………………………………………………………….

…………………………………………………………..

…………………………………………………………..

Namba ya simu……………………………………………………………………………………

Iwapo nitapata uhamisho au kubadili makazi, ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi.

Saini ……………………………. Tarehe……………………………

**NB: (Fomu hii irudishwe kwa Mkuu wa Shule ikiwa imejazwa)**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

Loleza Secondary School
P.O.Box 95,
MBEYA
………………

To
THE MEDICAL OFFICER,
……………………………..
……………………………..
……………………………..

Please examine…………………………………………………………
As to her fitness for pursuing further education at this school,

1. Haemoglobin ………………………………………………………………………………
2. P.V. Bleeding ……………………………………………………………........................
3. (a) Sight defect ……………………………………………………………………………………
   (b) Hearing…………………………………………………………………………………
4. Blood Pressure………………………………………………………………………………..
5. Urine for Sugar and Pregnancy test…………………………………………………………..
6. Stool for routine examination……………………………………………………………………………
7. Asthma………………………………………………………………………………………
8. Skin diseases…………………………………………………………………………………
9. Leprosy ………………………………………………………………………………………..
10. Epilepsy………………………………………………………………………………………
11. Pulmonary tuberculosis……………………………………………………………………….
12. Deformity………………………………………………………………………………..
13. Mental Problem………………………………………………………………………………

Comments………………………………………………………………………………………

### MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by the Medical Officer)
I have examined the above named and consider that she/he is mentally and physically fit for studies.

**Signature ……………………………………………………. Date …………………………………**

**Designation ………………………………………….. Station ……………………………...**

**NB: (Fomu hii irudishwe Kwa Mkuu WA Shule ikiwa imejazwa)**

## ORODHA YA VITABU MUHIMU KWA KILA SOMO

**Unashauriwa kumnunulia mwanao vitabu kulingana na masomo anayosoma. Orodha ya vitabu unavyoweza kumnunulia/vinavyotakiwa kwa kila idara ni kama ifuatavyo;**

### GENERAL STUDIES

1. General studies for Advanced level Certificate, Form Six (6) by Richard R.F. Mbalase (2011)
2. General studies for Advanced level Certificate, Form five (5) by Richard R.F. Mbalase (2011)
3. Contemporary approach for Advanced level "General studies Notes" Form 5 & 6 by Nyambari C.M. Nyangwine, Godfrey Rutta Nyangwine, Steven O. Maluka (New syllabus (2009).

### HISTORY

1. **History For Secondary Schools Form five & Six. By Tanzania Institute of Education.**
2. **Essentials in Advanced Level History Paper I & 2. By Saleh Yassin.**
3. Major issues in African History by Tanzania Institute of Education
4. History of Modern Europe by Peacock
5. How Europe underdeveloped Africa by W. Rodney
6. History in focus: Modern World History by Ben Walsh
7. Matering Advanced level History book two, by Kato, A (2011).
8. Matering Advanced level History book one, by Kato, A (2012)

### KISWAHILI

1. Kimbunga - H. Gora (Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili) (TUKI), 1994
2. Mapenzi Bora – S. Robert (Mkuki na Nyota)
3. Chungu Tamu – T.A. Mvungi (Tanzania Publishing House), 1985
4. Fungate ya Uhuru – M.S. Khatibu (MacMillan and Aidan)
5. Vuta N'kuvute – Shafi (Mkuki na Nyota 1999)
6. Kufikirika – S. Robert (Mkuki na Nyota 2003)
7. Mfadhiliwa – Hussein Tawa (Methew & Stationery 2007)
8. Usiku utakapokwisha – Mbunda Msokile 2007
9. Morani – E. Mbogo
10. Nguzo mama – P. Muhando
11. Kivuli kinaishi –
12. Kwenye ukingo wa Thim – E. Hussein
13. Kunga za Fasihi na Lugha – M. Msokile (1992)
14. Fasihi – F.E.M.K. Senkolo 1984
15. Kitangulizi cha tafsiri nadharia na mbinu – Mwansoko, H.J.M. (1996)
16. Nadharia ya Lugha kidato cha tano na sita – Suluhaya, M.C. (2

### GEOGRAPHY

1. **Physical Geography For Adavance Secondary Schools – form five & Six - By Tanzania Institute of Education.**
2. **Practical Geography For Adavance Secondary Schools – form five & Six - By Tanzania Institute of Education.**
3. **Human Geography For Adavance Secondary Schools – form five & Six - By Tanzania Institute of Education.**
4. **Principles of Physical Geography by Monkhouse (2008)**
5. **Research methodology, Methods and Techniques. By C. R. Cothari**.
6. Landforms in Africa by Collin Buckle
7. Map Reading by Mac Master
8. **Human and Economic Geography by C. Morgan (1982)**
9. **Geography, An integrated Approach; Fourth edition by David Waugh (2009)**
10. **Practical Geography for Africa by John M. Pritchard (1990)**
11. Map Reading, General Publications Ltd.- DSM by Durra, S.E.(2003)
12. R.B. Bunnet (2007) General Geography in diagrams.

### ENGLISH

1. **English Language for Secondary school s. Language and Language use. Form Five and six. By Tanzania Institute of Education.**
2. Macmillan Education Ltd.2000, Encounters from Africa, Macmillan
3. Ayi Kwei Amah, 1996, The Beautiful ones are not yet born, EAEP
4. Chinua Achebe, 1991, A Man of the People, BAEP
5. Ndunguru 1999, Divine Providence, Mkuki na Nyote
6. Magala Nyago, 1985, The Rape of the Pearl Macmillan
7. Namige Kayondo, 1995 Vanishing Shadows, Macmillan
8. Danny Sato, 1983, His Excellency the Head of State, Macmillan
9. David Omowale, 2002, A season of Welting, EAEP
10. Fransis Lubuga, 1990, Betrayel in the city, Heinemann
11. Ngugi wa Thiong'o, et al 1982, I will marry when I want, EAEP
12. Bukenya, 1984, The Bride, EAEP
13. Okot Omitah 1991, Lwanda Magere Heinemann
14. Henrik Ibsen, 1974, An Enemy of the people, Eyre Matheuen
15. John Ruganda 2005, Black Mamba, EAEP
16. Charles Mloka, 2002, The wonderful surgeon and other poems, Mkuki na Nyota
17. Tanzania Institute of Education, 1996, Selected Poems, Print Pak (T) Limited.
18. The real English textbook for Advanced level, Dr.Kadeghe Michael

**PHYSICS**

1. **Physics for Advanced Level Secondary schools – Student'S Book for Form Five and Six (Tanzania Institute of Education).**
2. Advanced level Physics 6$^{th}$edition by Nelkon and Parker (1989).
3. Advanced Physics by Tom Duncan
4. Advanced level Physics paper 1 and paper 2 by E. Njau (2002)
5. Principle of physics for class XII & XI by S.Chand (2011)
6. A-level Physics fourth edition by Roger Muncaster (fourth edition) (1993)

**MATHEMATICS**

1. Basic and Applied mathematics by **Respicius Kiiza (2010)**
2. Mathematics for class Xi & XII by DASS, H.K & VERMA, R. (2000)
3. Pure mathematics (revised edition) by M.F Macrae (2011)
4. Pure Mathematics **Volume 1 &2** by Backhouse, J.K (1985)
5. Core Mathematics for Advanced level by L. Bostock
6. Advanced level Mathematics by L.K. Shayo
7. Advanced level Mathematics Vol.1 & II by Kinunda (1974).

**BIOLOGY**

1. Dissecting kit
2. **Biology for Advanced Level Secondary schools – Student'S Book for Form Five and Six (Tanzania Institute of Education).**
3. **New understanding Biology for A-level student** by Glenn & s. Toole (1999)
4. Systematic and classification by L.K. Msaki (1993)
5. Biology, A functional Approach by M.B.V Roberts (1971)
6. Advanced Biology: Principle and Application by C.J. Clegg & D.G. Mackean (2000)
7. Biological Science by Taylor, etal (1997)
8. S. Chand's Biology for class XI & XII by P.S Verma & B.P Pandey (2005).
9. Guide to dissection by H.G.Q Rowett (2005)

**CHEMISTRY**

1. **Physical chemistry for Advanced Level Secondary schools – Student'S Book Form Five and Six (Tanzania Institute of Education)**
2. **Inorganic chemistry for Advanced Level Secondary schools – Student'S Book Form Five and Six (Tanzania Institute of Education)**
3. **Organic chemistry for Advanced Level Secondary schools – Student'S Book Form Five and Six (Tanzania Institute of Education)**
4. **General chemistry for Advanced Level Secondary schools – Student'S Book Form Five and Six (Tanzania Institute of Education)**
5. Advanced Chemistry Physical and industrial by P. Mathew (2006)
6. Essentials of physical chemistry by Arun Bahil, B.S Bahil & G.D Tuli (2012).
7. Organic Part **A & B** by A. Abdullah & M.H. Nkunya.
8. Inorganic **Part A & B** by J.S Maro Guterman & M. Mikesewala (1989)
9. Physical Chemistry by Ddungu& J.B.A Mihigo (1998)

10. Advanced level Inorganic Chemistry **PART I & II** by Tanzania Institute of Education (1995)
11. Organic Chemistry an introduction by Jack E. Fernandez (1982)
12. Understanding Chemistry for A-level student
13. Conceptual chemistry for class XII& XI by S.K Jaini (2011).
14. Advanced level chemistry, fourth edition by E.N Ramsden (2000)

**MIFANO YA AINA YA VITAMBAA**

1. **Aina ya Kitamba kwa ajili ya kushona sketi -bluu bahari (light blue)-kitambaa cha suti namba moja**



2. **Aina ya Kitamba kwa ajili ya kushona Gauni (shamba dress) – "DARK BLUE" – KITAMBAA CHA SUTI NAMBA MOJA**

